DAR RAPID TRANSIT AGENCY

# WAKALA WA MABASI YAENDAYO HARAKA




# FURSA ZA UWEKEZAJI KWENYE MRADI WA DART

**Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka - DART unakaribisha wadau wa maendeleo, makampuni ya ndani na ya kimataifa, pamoja na wajasiriamali wadogo na wa kati kuchamkia fursa za kiuchumi zinazopatikana katika ukuaji na upanuzi wa mradi huu mkubwa wa usafiri wa umma barani Afrika.**

**USAFIRI WA UMMA NADHIFU**

**Swali la kujiuliza ni kwanini Wawekezaji wanakaribishwa kuwekeza kwenye Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka? Zipo faida za kimkakati wa wawekezaji wote wakubwa na wadogo kama vile;**

i. **Soko la Uhakika:**
Jiji la Dar es Salaam linakua kwa kasi na linataraji wa kuwa Megacity (Watu zaidi ya milioni 10) ifikapo 2030. Uhitaji wa usafiri wa umma ni wa kudumu na unaongezeka kila siku.

ii. **Ulinzi wa Kisheria wa Uwekezaji:**
Tanzania ina mazingira imara ya kisera kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania na Mfumo wa Sekta ya Umma na Binafsi (PPP), unaolinda mitaji ya wawekezaji wa ndani na wa nje.

iii. **Miundombinu Iliyojengwa na Serikali:**
Watoa huduma katika Mradi wa DART, hawaingii gharama za kujenga barabara au vituo kwani Serikali imeshabeba gharama hizo kubwa, hivyo mwekezaji anajikita kwenye uendeshaji tu.










Kwa mantiki hiyo, Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka unawakaribisha wawekezaji kuja kuangalia fursa na kuwekeza kwa manufaa ya pande zote mbili. Fursa hizo zimegawanywa katika makundi mawili ya Wawekezaji wenye mitaji mikubwa na wale wawekezaji wenye mitaji midogo ambazo ni;

# KWA WAWEKEZAJI WENYE MITAJI MIKUBWA (NDANI NA KIMATAIFA)





**Hizi ni fursa** za kimkakati zinazohitaji ukwasi mkubwa wa kifedha, utaalamu wa hali ya juu, na uzoefu wa kimataifa, mara nyingi zikitolewa kupitia mfumo wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP) au zabuni za kimataifa ili kuwekeza katika;

## Uendeshaji wa Mabasi.

Kutokana na ujenzi wa Awamu ya Nne na Tano unaoendelea kwa kasi, na awamu nyingine zijazo kuna uhitaji mkubwa wa watoa huduma wa mabasi.

Watoa huduma hawa watahusika na ununuzi na uingizaji wa mabasi makubwa ya mita 18 na mabasi Mlishi ya mita 12. DART inawakaribisha wawekezaji kuingia mikataba ya uendeshaji ya muda mrefu wenye hakikisho la kureyesha mtaji uliowekezwa.

## Uwekezaji katika Nishati Safi na Mabasi ya Umeme.

Katika kuelekea uchumi wa kijani, DART inapanga kuachana kabisa na mabasi ya dizeli na kwani kwa sasa imeanza kutumia mabasi yanayotumia Gesi Asilia (CNG) na hapo baadaye ikipanga kutumia pia mabasi ya Umeme. Hivyo ipo fursa ya uwekezaji katika ujenzi na uendeshaji wa miundombinu ya kuchaji mabasi ya umeme, mifumo ya usambazaji wa gesi asilia kwenye karakana za mabasi, na uingizaji wa teknolojia rafiki wa mazingira.



## Maendeleo ya Maeneo ya Vituo.

Vituo vikuu vya DART (kama Kimara, Mbagala, Morocco, na Gerezani) vinapitiwa na mamia ya maelfu ya watu kila siku. Maeneo yanayozunguka vituo hivi yana thamani kubwa ya kiuchumi. Fursa ya uwekezaji katika eneo hili ni ujenzi wa majengo makubwa ya kibiashara, hoteli za wasafiri, maghala ya mizigo, na majengo ya maegesho ya ghorofa jirani kabisa na miundombinu ya DART.




**Mifumo ya TEHAMA na Ukusanyaji Nauli.**

Mfumo wa DART una uhitaji wa mifumo thabiti na salama ya usimamizi wa mabasi. Hivyo uwekezaji unahitajika katika ushirikiano wa kukuza mifumo ya kisasa ya ulinzi wa data, mageti ya kisasa, na mifumo ya kadi zinazoweza kusomeka kimataifa.

---

**Viwanda vya Kuunganisha Mabasi nchini.**

Kila awamu mpya ya Mradi wa DART inapokamilika, mamia ya mabasi mapya yanahitajika. Kuagiza mabasi yaliyokamilika kutoka nje ya nchi kunachukua muda mrefu na kuongeza gharama za usafirishaji na kodi. Hivyo makampuni makubwa ya kimataifa ya utengenezaji wa magari yanakaribishwa kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vya kuunganisha mabasi hapa nchini Tanzania. Uwekezaji huu unafungua soko la uhakika la kuuza mabasi kwa makampuni watoahuduma katika mradi wa DART, na pia kusambaza kwenye miradi mingine ya Mabasi Yaendayo Haraka inayochipukia nchi za jirani barani Afrika.





## Uwekezaji kwenye Mifumo ya Data na Akili Unde.

Mfumo wa DART unazalisha mamilioni ya data kila siku kama vile muda mabasi yanapotembea, maeneo yenye foleni, mwenendo wa safari za abiria nyakati za asubuhi na jioni, tabia za abiria za ukataji tiketi, nk. Data hizi bado hazijatumika kikamilifu kibiashara. Hii ni fursa ya uwekezaji kwa makampuni makubwa ya teknolojia kuwekeza kwenye mifumo ya uchambuzi na Akili Unde ili kusaidia kuboresha ratiba za mabasi kiotomatiki kulingana na mabadiliko ya hali ya hewa au foleni, uuzaji wa data zilizochujwa kwa makampuni ya bima, mabenki, na wataalamu wa miji.




## Uwekezaji wa Karakana za Kisasa na vituo vya matengenezo ya mabasi.

Kwa mfumo wa Ubia katika ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP), wawekezaji wanakaribishwa kuja kujenga na kusimamia Karakana za Kisasa zenye mifumo ya kiotomatiki ya kuosha mabasi kwa kutumia maji yanayoweza kutumika tena, mifumo ya kisasa ya maghala ya vipuri, na karakana za matengenezo makubwa ya injini na mifumo ya umeme ya mabasi pamoja na gesi.



# KWA WAWEKEZAJI WENYE MITAJI YA KATI NA MIDOGO




Fursa hizi zimewekwa mahususi ili kukuza uchumi wa ndani, zikiwalenga wafanyabiashara wa Kitanzania na wajasiriamali wadogo na wa kati ambao wanataka kutumia mfumo wa DART kujipatia kipato. Fursa hizo ni;

Ukodishaji wa maeneo ya biashara ndani ya vituo. Ndani ya vituo vikuu na vidogo kuna nafasi maalum zilizotengwa kwa ajili ya biashara za huduma za kila siku kama vile ufunguzi wa maduka ya kahawa, vinywaji, na vyakula vya haraka. Maeneo ya kuweka mashine za benki za kutolea fedha na vibanda vya mawakala wa huduma za kifedha. Aidha, wawekezaji wanakaribishwa kufungua maduka madogo ya magazeti, vitabu, dawa, na mahitaji madogo ya wasafiri.




**Fursa ya Matangazo ya Biashara.**

Uwepo wa abiria zaidi ya 200,000 kwa siku katika Awamu ya Kwanza pekee ni fursa kubwa kwa mashirika na makampuni ya utangazaji kufikia wateja. Makampuni ya ndani ya uwakala wa matangazo yanakaribishwa kukodi nafasi za matangazo kwenye kuta za vituo, madaraja ya juu ya watembea kwa miguu, skrini za kidijitali za vituoni, na kubandika matangazo ndani na nje ya mabasi.

**Huduma za Ulinzi, Usafi, na Matengenezo.**

Ili miundombinu ya mfumo wa DART ibaki katika ubora wa hali ya juu, Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka unatafuta makampuni binafsi ya kutoa huduma saidizi kwenye eneo kusafisha vituo na barabara za Mabasi Yaendayo Haraka, ulinzi wa miundombinu na vifaa vya kituo saa 24, uendeshaji na usimamizi wa huduma za vyoo vya umma vilivyopo vituo vikuu pamoja na matengenezo ya miundombinu na vifaa vya mradi wa DART.



## Huduma ya Maegesho Salama.

Mfumo wa DART unao fursa ya wasimamizi wa maeneo ya kuegesha magari, pikipiki na baiskeli za abiria wanaotumia Mabasi Yaendayo Haraka kwenye vituo vya kati na pembezoni. Wawekezaji wa ndani wanakaribishwa kuingia ubia na Wakala wa DART kusimamia maeneo haya ya maegesho kwa kuweka mifumo ya kisasa ya kutoa risiti, ulinzi wa kamera, na ukusanyaji wa ushuru wa maegesho kibiashara.

---

## Urejelezaji wa Taka za Miundombinu.

Mradi wa DART unazalisha taka nyingi zinazoweza kurejelezwa na kugeuzwa kuwa fursa ya kibiashara. Fursa zake za uwekezaji katika ni Wajasiriamali wa ndani kuja kuingia mikataba na Wakala wa DART au Watoa Huduma katika mradi kwa ajili ya; Kukusanya na kurejeleza matairi chakavu ya Mabasi Yaendayo Haraka na kuyageuza kuwa bidhaa nyingine kama vile vifaa vya michezo, mazulia, au viatu. Vilevile kukusanya betri chakavu za mabasi (hasa yanayokuja ya umeme) na mafuta machafu ya injini yaliyotumika kwa ajili ya usafishaji salama wa kimazingira.





# WASILIANA NASI

Ubungo Maji, Morogoro Road
S. L. P 724, Dar es Salaam
Simu: + 255 22 2922 8634/33
Fax: + 255 22 92 8635
Email: info@dart.go.tz
au mteja@dart.go.tz

DARTmwendokasi    DARTTV

*Usafiri wa Umma Nadhifu*

DART
DAR RAPID TRANSIT AGENCY